**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# SCHOOL BASED ASSESSMENT

**KISWAHILI SEHEMU A**

## Gredi ya 8

## NAKALA YA MWALIMU

**SEPTEMBA 2024**

**© KNEC 2024** **Geuza ukurasa**

**Sehemu A inatathmini stadi ya Kusikiliza na Kuzungumza. Inajumuisha mazoezi mawili:**

**Zoezi 1: Kusikiliza na Kuzungumza**

i. Mazungumzo ya ana kwa ana

ii. Ufahamu wa Kusikiliza

**Zoezi 2: Kusoma**

i. Kusoma kwa sauti

**MUDA: Dakika 15 kwa kila mwanafunzi.**

**Maagizo ya jumla**

1. Mwalimu awafahamishe **wanafunzi wote** kwamba mazoezi yote katika sehemu hii yatakuwa ya ana kwa ana. Kila mwanafunzi atakuwa na zamu yake ya kutathminiwa; mmoja baada ya mwingine.
2. Mwalimu awafahamishe wanafunzi wote kwamba karatasi hii ina mazoezi mawili.
3. Mwanafunzi aandaliwe kiti au dawati kutazamana na mwalimu.
4. Mwalimu atangulize kila zoezi na amfahamishe mwanafunzi matarajio ya kila zoezi.
5. Mwalimu amfahamishe mwanafunzi kukamilika kwa kila zoezi.
6. Mwalimu atathmini umilisi wa mwanafunzi kwa mujibu wa mwongozo wa kutathminia pamoja na kuweka rekodi.

# ZOEZI 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

## ZOEZI IA: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA

**Maagizo maalum**

i. *Andaa mazingira mazuri ya tathmini kwa kumkaribisha mwanafunzi.*

ii. *Mwamkue na kumwomba akae.*

iii. *Jitambulishe kwake kwa kusema, 'Mimi ni mwalimu________________'.*

iv. *Muulize jina lake.*

v. *Anza tathmini kwa kusema,*

"Usafi ni muhimu katika maisha yetu. Ningependa tuzungumze kuhusu usafi wa sehemu za umma."

1. Hebu nitajie sehemu mbili za umma unazozifahamu?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

2. Baadhi ya wenzako hawazingatii usafi wa sehemu za umma. Utawashauri vipi?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

3. Umetembelea soko lililo karibu na kwenu. Umegundua kwamba soko hilo ni chafu. Je, utafanya nini ili kubadilisha hali hii?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

**4.** Panapokuwa na watu wengi sokoni tunasema pana umati wa watu. Je, panapokuwa na taka nyingi tutasemaje?
   **(Mwanafunzi ajibu)**

**Geuza ukurasa**

**ZOEZI IB: UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

**Maagizo maalum**

i. *Msomee mwanafunzi kifungu kifuatacho* ***mara mbili.***

ii. *Mjulishe kuwa atajibu maswali baada ya kusomewa kifungu mara ya pili.*

Ukosefu wa usalama ni changamoto katika baadhi ya maeneo nchini mwetu. Kila uchao visa vya uhalifu huripotiwa kwenye redio, runinga na hata katika mitandao ya kijamii. Hali hii imewasababishia wananchi madhara si haba. Je, kudumishwa kwa usalama ni jukumu la nani?

Yeyote anayeshuhudia kisa cha uhalifu anastahili kupiga ripoti kwa idara zinazohusika. Kufanya hivyo kutawezesha hatua mwafaka kuchukuliwa ili kukomesha kutokea kwa kitendo kama hicho. Vilevile, wananchi wanashauriwa kuwafahamu wale wanaoishi karibu nao kuambatana na mpango wa serikali wa 'Nyumba Kumi'. Kwa njia hii, itakuwa rahisi kuwatambua na kuwaripoti wahalifu.

Pengine unajiuliza kwa nini ni muhimu kwa wananchi kuzingatia usalama. Mengi yanaweza kupatikana nchi inapokuwa na usalama wa kutosha. Wafanyabiashara wataendesha shughuli zao bila wasiwasi, watoto watapata elimu, wafanyakazi nao watatenda kazi zao kwa amani na nchi itapiga hatua kimaendeleo. Hii ndiyo maana sote tunapaswa kushikana mikono ili kuhakikisha usalama unadumishwa kote nchini. Ikumbukwe umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.

5. Ni changamoto gani ambayo huripotiwa kwenye vyombo vya habari?
**(Mwanafunzi ajibu)**

6. Kulingana na kifungu, uwajibikaji wa kila mmoja wetu utachangia vipi kudumishwa kwa usalama?
**(Mwanafunzi ajibu)**

7. Unadhani ni nini kitatendeka uhalifu usipokomeshwa?
**(Mwanafunzi ajibu)**

**8.** Kauli, **'**kushikana mikono' imetumiwa kwenye kifungu. Kushikana mikono ni kufanya nini?
**(Mwanafunzi ajibu)**

**ZOEZI 2 : KUSOMA KWA SAUTI**

**Maagizo maalum**

i. *Mfahamishe mwanafunzi matarajio ya Zoezi la Kusoma. (Zingatia mwongozo wa kutathminia kusoma kwa sauti).*

ii. *Mpe mwanafunzi nakala atakayoisoma kwa sauti.*

iii. *Mwanafunzi anaposoma, sikiliza na kurekodi idadi ya maneno anayosoma kwa muda wa* ***dakika moja.***

iv. *Onyesha kwa mshazari* ***(/)*** *mahali mwanafunzi alipofikia kusoma* ***dakika moja*** *ikikamilika.*

v. *Mruhusu mwanafunzi kusoma mpaka mwisho wa kifungu.*

vi. *Pigia mstari maneno* ***yote*** *ambayo mwanafunzi atashindwa kuyasoma au kuyatamka vizuri.*

vii. *Rekodi idadi ya maneno ambayo mwanafunzi ameweza* ***kusoma kwa usahihi*** *kwa dakika* ***moja****. (Baada ya kuondoa yaliyotamkwa vibaya au/na aliyoshindwa kutamka)*

viii. *Rekodi viwango vya umilisi wa mwanafunzi kwa kuzingatia mwongozo uliopewa.*

ix. *Hakikisha una nakala ya kurekodia tathmini hii. (Iwe na majina ya wanafunzi wote.)*

x. *Ukiwa tayari kuanza tathmini, sema,*

‘‘Sasa naomba unisomee kifungu hiki kwa sauti.’’

**Mwalimu amwambie mwanafunzi asome kifungu kifuatacho kwa sauti.**

Mtu anapougua hutafuta matibabu kutoka kwa daktari. Kwa kawaida, daktari[10] humwandikia mgonjwa huyo dawa zifaazo baada ya kumfanyia uchunguzi. Inatarajiwa[20] kwamba mgonjwa akishaandikiwa dawa atazitumia kulingana na maagizo. Asipofanya hivyo,[30] huenda dawa hizo zikakosa kufanya kazi iliyokusudiwa au hata kumdhuru.[40]

Zipo dawa za aina mbalimbali. Kuna zile ambazo humezwa, za[50] kutiwa kwenye sehemu zenye maumivu, za kupakwa na hata za[60] kudungwa kwa kutumia sindano.

Ili kuhakikisha matumizi yafaayo ya dawa,[70] jamii inashauriwa kuzingatia maagizo ya daktari. Kwa mfano, kutumia dawa[80] kwa viwango vilivyopendekezwa, kuzitumia kwa wakati ulioagizwa na kutowapa wagonjwa[90] wengine dawa zako. Isitoshe, tunafaa kuongeza kiasi cha maji kinachofaa[100] kulingana na maelekezo yote yaliyotolewa.[105]// Tufahamu kuwa si vyema kununua dawa bila ushauri wa daktari. [115]

Aidha, wanajamii wanatahadharishwa dhidi ya kuweka dawa ovyoovyo. Inastahili kuzihifadhi [125]mahali palipo salama na mbali na watoto.[132]

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**